HABARI KITAIFA

Ndaki acharuka mnada kukosa mapato miaka 4

Na Halima Ikunji, IGUNGA

WAZIRI wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewasimamisha kazi msimamizi wa mnada wa Igunga mkoani Tabora, Juma Athumani, kwa tuhuma za ubadhilifu wa fedha na ametoa maelekezo kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kuondolewa Ofisa Afya ya Mifugo, Mohamed Kifamba.

Pia, amemtaka Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Igunga, kuwaondoa askari polisi waliokuwa wakisimamia mnada huo kutokana na tuhuma za ubadhirifu.

Ndaki alichukua hatua hiyo jana wakati wa ziara yake katika mnada huo baada ya kubaini kutokuwapo nyaraka za kumbumbuku za tozo na mauzo ya mifugo walioingia na kutoka katika mnada huo kwa muda wa zaidi ya miaka minne.

Waziri huyo alisema kwamba kukosekana kwa kumbukumbu hizo kumeishababishia serikali hasara ya fedha nyingi jambo ambalo haliwezi kuvumilika. Alisema licha ya kuwasimamisha kazi watuhumiwa hao alivitaka vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma za ubadhirifu wa mapato ya serikali yaliyopotea kwa kipindi cha miaka minne.

"Nasema haiwezekani, haiwezekani serikali haiwezi kuvumilia kuendelea kukosa mapato wakati kila siku ya minada inapofanyika na watu wachache wakiiba," alisema Waziri Ndaki.

Amemwagiza Katibu Mkuu wizara yake, kupeleka watu wa ukaguzi na kufanya uchunguzi wa kina kwa ajili ya kuangalia mapato ya serikali yaliyopotea katika kipindi hicho.

Pia, alimsimamisha kazi msimamizi wa mnada huo, Haidari Mwinyihija, kuendelea kuuangalia mnada huo wakati serikali ikiendelea na utaratibu wa kumpata mtu mwingine wa kufanya kazi hiyo.

Waziri Ndaki alimtaka Mkurungezi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, kupeleka ofisa mifugo mwingine na mkuu wa polisi wa wilaya hiyo kupeleka askari wengine katika mnada huo.

Vyam

Na Deogratius Nsc
KIBONGO

Vyama saba vya kumi vilivyochuk gombea ubunge l la Muhamwe wilay Mkoa wa Kigoma, kukidhi vigezo vy ubunge katika kati mdogo wa ubung wa takaofanyika M huu.

Vyama ambavy vigezo na wagombe teuliwa ni Julius Ma Wazalendo, Dk. Flo wa CCM na Philipo Democratic Party (D

Msimamizi wa uc

Naibu Waziri wa Ha Manyara, akizungu
PICHA: GIFT THADE

Scanned with CamScanner

Daily News Uk. 18, Tarehe
06/04/2020



FISHERMEN socialize before going for fishing at Magogoni Fish Market in Dar es Salaam yesterday.(Photo by Mohamed Mambo)

Scanned with CamScanner

Msimamizi wa mnada Igunga atumbuliwa

Na Allan Vicent, Igunga

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amemsimamisha kazi ofisa anayesimamia mnada wa mifugo wa Upili ulioko wilayani Igunga mkoani Tabora, Juma Athuman kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za mapato...Inaendelea Uk. 4

Scanned with CamScanner

(Brazil), Ecopetrol (Colombia),

Msimamizi wa mnada Igunga atumbuliwa

Na Allan Vicent, Igunga

■■WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amemsimamisha kazi ofisa anayesimamia mnada wa mifugo wa Upili ulioko wilayani Igunga mkoani Tabora, Juma Athuman kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za mapato.

Waziri alichukua hatua hiyo juzi alipotembelea mnada huo ili kuangalia ufanisi wake, ambapo alibaini kutokuwepo nyaraka za kumbukumbu ya mifugo inayoingia na kutoka katika mnada huo kwa kipindi cha miaka 4 mfululizo.

Alisema kukosekana kwa kumbukumbu hizo kumetoa mwanya wa upotevu wa mapato ,hivyo kuisababishia Serikali hasara ya mamilioni ya fedha, hivyo jambo hilo halikubaliki hata kidogo.

'Naagiza Uongozi wa Halmashauri kumwondoa kazini mara moja Ofisa Afya ya Mifugo, Mohamed Kifamba na askari polisi wote waliokuwa wakisimamia mnada huo nao waondolewe mara moja," OCD shughulikia hilo', alisema.

Licha ya kusimamishwa kazi watuhumiwa hao Waziri aliagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina juu ya tuhuma hizo za ubadhirifu wa mapato ya serikali kwa kipindi chote cha miaka 4 ili sheria ichukue mkondo wake.

'Kila siku ya mnada fedha nyingi zinakusanywa, lakini hazionekani, zinaingia mifukoni mwa watu, hili halikubaliki na Serikali haiwezi kufumbia macho vitendo vya namna hiyo kwa kuwa vinaikosesha mapato mengi sana," alisema Waziri.

Alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kupeleka wataalamu wilayani humo ili kuchunguza mapato ya mnada huo yaliyopotea katika kipindi chote hicho ili hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa ikiwemo wahusika kulipa fedha hizo.

Aidha waziri huyo alichukua ya kumkaimisha msamamizi wa mnada huo, Haidari Mwinyihija kuendelea kuungalia mnada huo

Wakati utaratibu wa kumpata ofisa mwingine atakayesimamia mnada huo ukiendelea kufanyika, Waziri alimteua Haidari Mwinyihaji kusimamia mnada huo kwa muda.

Waziri Ndaki alimtaka Mkurungezi wa Halmashauri hiyo kupeleka haraka Mtaalamu mwingine atakayesimamia mifugo katika mnada huo, huku akimtaka OCD wa wilaya hiyo naye kupeleka askari wengine.

Scanned with CamScanner

Waziri Ndaki amtumbua msimamizi wa mnada kwa ubadhirifu

NA BENNY KINGSON, IGUNGA

OFISA anayesimamia mnada wa mifugo wa Upili uliopo Wilayani Igunga Mkoania Tabora Juma Athumani amesimamishwa kazi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za mapato.

Waziri Ndaki amechukua hatua hiyo juzi alipotembelea mnada huo ili kuangalia ufanisi wake ambapo alibaini kutokuwepo nyaraka za

kumbukumbu ya mifugo inayoingia na kutoka katika mnada huo kwa kipindi cha miaka 4 mfululizo.

Alisema kukosekana kwa kumbukumbu hizo kumetoa mwanya wa upotevu wa mapato hivyo kuisababishia serikali hasara ya mamilioni ya fedha, jambo hili halikubaliki hata kidogo.

"Naagiza Uongozi wa Halmashauri kumwondoa kazini mara moja Ofisa Afya ya Mifugo Mohamed Kifamba na askari polisi wote waliokuwa wakisimamia mnada huo nao waondolewe mara moja, OCD shughulikia hilo," alisema.

Licha ya kusimamishwa kazi watuhumiwa hao Waziri huyo aliagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina juu ya tuhuma hizo za ubadhirifu wa mapato ya serikali kwa kipindi chote cha miaka 4 ili sheria ichukue mkondo wake.

"Kila siku ya mnada fedha nyingi zinakusanywa lakini hazionekani, zinaingia mifukoni mwa watu, hili halikubaliki na Serikali haiwezi kufumbia macho vitendo vya namna hiyo kwa kuwa vinaikosesha mapato mengi sana," alisema.

Scanned with CamScanner